## SURA YA KWANZA

## KANISA NI NINI?

Katika maisha kuna maana na tafsiri ni vitu vinavyoweza kuleta mkanganyiko na vinaendelea kuleta mkanganyiko kanisa kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri kulingana na taarifa alizopokea katika mapokeo yake.

Ila maana ya kanisa ni sehemu ya watu kukutana nakuabudu kanisa haina maana ya jengo inaweza kuwa mahali popote pale mahususi kwa watu kumuabudu mungu,

Hiyo nimaana ya kawaida kwa mtu kuelewa lakini swali hili lina uchambuzi ambao haujalenga hasa katika maana ya kanisa kama tulivyoona hapo awali, tunajaribu kuona kanisa kwa maana ya yaliyomo katika imani za watu kupitia nyumba za ibada hasa makanisa.

Dhana ya makanisa na kusudi la kanisa je ndiyo ilivyo sasa? mioyo ya watu ambao tunaoweza kuhisi niwaamini wazuri ikoje? vipi kuhusu tafsiri za watu wao kwa wao katika kanisa zinaendana na vile Yesu kristo alivyo wahasa watu kuenenda?

### Kusudi la kanisa

kusudi la kanisa ilikuwa nikuwaunganisha watu pamoja bila kuangalia hali walizonazo kimaisha, dhumuni au kusudi la kanisa nikuwafanya wakristo kuwa kitu kimoja nakusaidiana hasa kwa watu wenye maisha magumu katika wigo mbalimbali,

kiujumla hayo ndiyo yalikuwa makusudio ya kuanzisha makanisa hususani ya kikatoriki duniani sambamba na kuinjrisha injiri kwa watu nakuijuwa kweli kuhusu neno la mungu.

Kanisani nisehemu ambayo inamatarajio ya watu kupata faraja hasa kwa wale waliokata tamaa za maisha inaweza kuwa kimbilio, Tafiti zinaonyesha watu hasa wa imani ya kikristo wana fikra thabiti kuhusu kanisa ndiyo maana hakuna watu wenye siri nyingi za watu kama viongozi wa kanisa na makasisi n.k.

Inakuwa hivyo kutokana na jinsi watu wanavyo waamini kama viongozi wao wa kiroho upande wa viongozi hawa wakiroho hauna changamoto nyingi ukilinganisha na watu wanao walea katika imani,

Tunapoingia kanisani tunaona watu wengi wakiwa wamekaa wakiangalia Altare bilashaka katika muktadha wa kawaida tunaweza kusema niwatu sawa na wenye lengo moja na kusikilizana sambamba nakuchukuliana.

kuchukuliana ikiwa na maana kanisani watu wote hawawezi kuwa na akili sawa wala mitazamo sawa kuna watu wenye tabia nakasumba tofauti je watu wanachukuliana katika mapungufu watu walio nayo ndani ya kanisa?

Ukweli nikuwa kuna mikanganyiko mingi utafiti wa kiuwandishi unaonyesha makanisani ndiko kumetawaliwa na hali ya kuyaona makosa ya mwingine kuliko yale mtu aliyonayo au (Mapungufu binafsi).

Kanisani ndiyo sehemu ambayo watu wanahukumiana kwa haraka kuliko sehemu nyingine za kawaida inakuwa hivyo kutokana na watu wengi kushindwa kuelewa ibirisi yuko ndani yakanisa pia kila unapotoa mguu nae yupo yakupasa kuwa na umakini wa hali ya juu kama mkristo kuelewa suala hili ndiyo maana siku hizi sio jambo geni kuona ndani ya kanisa watu wakisengenyana wakisemana vibaya,

Wengine huwenda mbali nakuhukumu waumini wenzao bila hata ya kujuwa kweli zao kuhusu maisha binafsi ambayo wanapitia.

Ukweli kuhusu kanisa nikueneza upendo mapadre n.k. wanafanya hivyo kwa kiasi wanavyoweza nakusikiliza watu lakini hali ikoje kwa wanao waongoza kiimani?

Hapa kuna tatizo kubwa tunapo zungumzia kanisa tuna mzungumzia Yesu kristo aliye hai ambaye alikuwa amejawa upendo usiokuwa wakawaida upendo huwo wa Agape ndiyo unatakiwa kutafasirika kwa wanadamu wote duniani,

upendo kwa unaye mjuwa na usiye mjua je hii ndiyo taswira iliyopo katika kanisa lako? Kanisa si jengo kanisa ni pamoja nawewe na nafsi yako.

Yesu Kristo anapenda ukweli na ndiyo maana alihubiri ukweli nakueneza ukweli lakini kanisani kwa sasa kumejawa na vitu vingi ambavyo anapotokea mtu mwenye imani isiyo kamili anaweza kuacha kusali kutokana na matendo ya baadhi ya waumini waliojitafsiri kwa maneno kuliko matendo yenye huruma na unyoofu tunaweza kuwa sawa katika tafsiri lakini kimaana imani bado ikawa haionekani ndani ya matendo ya watu.

**Ukristo unamaana gani?**

nikuishi maisha sawa na aliyo yaishi Yesu kristo ambae tunaamini kupitia yeye ulimwengu umekombolewa kutoka katika utumwa wa dhambi nivyema kuishi maana kuliko tafsiri wakristo wengi wanaiishi tafsiri.

Ndiyo maana wanajikuta kuanguka nakwenda kinyume cha maana ya ukristo maisha ya mwanadamu hata adanganye vipi kwa maneno nakuigiza matendo yake yanaweza kuongea uhalisia kuhusu yeye.

Kanisa halina maana kama ikiwa matendo ya watu yatakuwa mabaya unyenyekevu katika madhabau hautoshi katika kuishi maisha ya kikristo bali unahitajika unyenyekevu wa kweli katika matendo ya kila siku,

unaweza kujiuliza nikwa nini makanisa yanakuwa mengi lakini dhambi hazipunguwi? na je wanaotenda dhambi ni akina nani? Na niwatu wanao amini au wasio amini? Kuna vitu vingi vyakujiuliza nakujitafakarisha kama mkristo,

Kinachofanyika niwatu kuingia makanisani kimazoea au kutafuta suluhu ya matatizo kwa haraka si kuishi ukristo tunapo zungumzia juu ya habari ya kuishi ukristo nikutenda matendo kama Yesu kristo maana ndiye mtu aliye mfano kwetu.

kristo hakuwa na majivuno kristo hakuwa mtu wakujikweza lakini kanisani kuna watu wanamajikwezo nabado wanajitafasiri kama wa kristo, ukristo sio salamu bwana asifiwe na tumsifu yesu kristo n.k. matendo ya watu wengi waliondani ya kanisa hayaendani na ukristo kinacho hubiliwa na matendo nivitu viwili tofauti,

Waumini wengi wanataka miujiza kuliko kujuwa ufalme wa mungu dunia ya sasa imejikita katika miujiza nakujikuta watu wamesahau yakuwa ukifahamu ukweli kuhusu ufalme wa mungu miujiza mingi inaweza kutokea hata pasipokutumia vitu kama kukanyaga mafuta n.k.

ukishakuwa mtu wakuangalia miujiza hutaweza kuushi ukristo hutaweza kuishi maisha sawa naya Yesu utakuwa unamtafuta Yesu usiye mjuwa watu wanao hangaika na miujiza wana tafuta kitu wasicho kijuwa huwo ndio uhalisia,

Isikimbiliwe miujiza haiwezi kusaidia kitu chochote kama watu wengi wanavyozani ukiwa mtu wa miujiza unaweza kuhangaika na makanisa mengi kuliko ilivyo kawaida.

kimsingi utakachokuwa unakitafuta hukijui ingawa katika tafsiri uliyonayo unaweza kuhisi uko katika usahihi Yesu kristo anaye hubiriwa sasa tofauti na kusudi lake unapochunguza makanisa mengi na ajenda zake nikama yesu anayetamkwa niwa kutenda miujiza yesu wa uponyaji nikweli yesu aliponya watu lakini nikwa namna gani na mtindo gani aliyotumia?

Umakini unahitajika katika maana ya ukristo sio katika tafsiri ya ukristo watu wanautafasiri ukristo vibaya kitu ambacho kinaendelea kufanya ulimwengu usibadilike ingawa kuna makanisa mengi yenye ajenda ya Yesu,

Ndani ya makanisa kuna utengano kiuhalisia wale wenye nacho ndio wanapewa nafasi katika safu za uwongozi asiye kuwa nacho anakuwa muumini wa kawaida wakutoa sadaka nakusikiliza neno mbaya zaidi nae hajui anacho kiabudu ni nini yuko kwenye (pazzle) yani fumbo.

Yesu mwenyewe alikaa na watu walio dhalaurika watu wachini aliishi maisha yasiyokuwa yakitajiri maisha ya kawaida,

Nilazima kila kinachofundishwa kanisani tukilinganishe na maisha ya kristo kanisa katoriki lina mfano mzuri wa watakatifu jinsi walivyoishi maisha ya taabu na misukosuko mingi.

Mfano wa hao watakatifu moja wapo ni mtakatifu Josephine Bakita mtakatifu mwafrika aliyeteseka na badae kuja kuwa mtawa matendo yake yalikuwa yakirandana na ukristo,

Mtakatifu Ritha Wakashia n.k. hawa kanisa katoriki limewachukua kama mifano kwa maisha yao walioishi jiulize mkristo hapo ulipo kwa kuendekeza miujiza itakufikisha wapi? watakatifu hawa na wengine ambao tunaweza kuwaona badaye hawakuwa wakiishi kwakutafuta miujiza waliishi maisha ya kikristo.

Maisha ya ukristo bila matendo sawa na aliyokuwa akifanya yesu nikazi bule unaweza kwenda kanisani ukaona kama tunapiga hatua lakini hatua zisiwe na maana katika ufalme wa mbingni.

kristo Yesu hakuwa mtu ambae aliyekuwa akinyooshea vidole watu hata kama walikuwa wadhaifu mkristo yoyote atakuwa anakamilisha ukristo wake kwakuyaishi maisha sawa na aliyoyaishi Yesu upole kujishusha na kujitoa kwa wengine,

Yesu aliponya watu biblia kitabu kitakatifu kinaonyesha hivyo hakuwa nahali ya kujitangaza jiulize je leo watu wanao ponya watu kwanini ifikie hatua ya kujitangaza?

Ukristo wa sasa hauna mantiki ile iliyokuwa imekusudiwa matendo yaliyomo katika kanisa na kile kilichokusudiwa imekuwa vitu tofauti Yesu anae hubiriwa amekuwa yesu wa vitu si Yule ambae watu wanatakiwa kuyachukua maisha yake nakuyatafsiri katika matendo.

ukweli wa kristo unahubiriwa kwa uchache kwasasa dunia ilipofikia haiitaji manabii wengi wakutenda miujiza bali inahitaji kuwa na walimu wengi wakufundisha nakuwafanya watu kufahamu ufalme wa mungu na jinsi unavyofanya kazi,

Huwo utakuwa msaada mkubwa kwa watu kuweza kujifaidi wenyewe nakuishi matendo ya kristo aliyo yafanya kama mfano tunaotakiwa kuishi.

Kwakuwa kanisa limesha kuwa nisehemu ya vitu vingi ambavyo nikinyume ndiyo maana matendo yale tuliyokuwa tukiyaona akifanywa na Yesu kristo hayapo badala yake kanisa unaweza kulitafasiri kwa namna nyingi,

inakuwa hivyo kutokana nakuwa na mafundisho yamejawa na tafsiri nyingi kuliko maaana watu wengi hawafundishwi maana kama ilivyokuwa maana ya kanisa na kusudi lake tafsiri zimekuwa nyingi makanisa yametofautiana jinsi ya utoaji wa neno la mungu ikiwa mungu ni moja na sote tuna hubiri juu ya habari ya Yesu aliye hai na mkombozi wa wanadamu kwanini makanisa ya tofautiane mafundisho?

Ukristo bilashaka unaweza kutofautiana unatofautina sikwa maana bali kwa tafsiri ya kila mmoja anayokuwa nayo kutokana na mapokeo aliyokwisha lishwa je fedha zinazotolewa makanisani nimsaada kwa wenye shida?

Ikiwa zinawafikia mbona wenye shida niwengi mitaani? Yesu alikuwa akiishi na watu wenye shida walikuwa ndiyo watu aliokuwa akitembea nao nakuwatembelea leo unaweza kuona watumishi au makuhani wakiishi maisha mazuri kuliko waumini wao hii inatafsiri gani na uhalisia gani katika maisha ya ukristo?

Si ajabu kukuta mtu mwenye shida akaachwa nakupuuziwa shida zake lakini mtu akaenda kutoa sadaka, Mambo kama hayo yanaonyesha wazi kwakiasi gani tuko katika hali ambayo huyaoni matendo ya kikristo hata katika fikra za watu,

Yesu mbinguni alipo na siku atakaporudi tunaweza kushuhudia vitu tofauti na vile ambavyo tunazania kutokana na kile kinachoendelea sasa duniani wingi wa makanisa ulitakiwa kubadilisha watu nakuwa na matendo mema yenye staha kama alivyokuwa akifanya kristo mokozi.

kutokana na vitu vingi kuwa kinyume unaweza kuona makanisani ndiyo sehemu yenye watu wenye matatizo mengi kuliko watu walio nje ya kanisa haimanishi watu wasihudhulie makanisani lahasha,

**Kwanini watu wengi hawaishi sawa na alivyokuwa Yesu?**

Maisha aliyo yaishi kristo ilikuweza kuyaishi hayahitaji miujiza yanatakiwa kulijuwa neno la mungu peke yake inatosha utalijuwa neno lake kwakujifunza, ndio maana hapo awali tumeona tunatakiwa kuwa na walimu zaidi wakufundisha neno nasio manabii na makuhani katika uponyaji wa miujiza.

ukilijuwa neno miujiza iko ndani yako imani yako itakuwa utajuwa mahusiano yako na mungu yanatakiwa jawe katika mfumo upi?

Ajenda nyingi katika kanisa zimekuwa si zakuwafanya wakristo kuhuwiwa na nguvu ndani yao ya kuyafuata matendo aliyo yafanya Yesu, si ajabu kukuta mkristo akiwa yuko kanisani lakini haguswi na shida ya mwingine.

si ajabu kukuta ndani ya kanisa kuna masengenyo na kuhukumu watu chuki n.k. unaweza kujiuliza sehemu kama hizo ukalinganisha matendo ya Yesu na kile unacho kiona unakosa uhalisia,

Watu kuishi maisha ya kristo inaweza kuwa vigumu kutokana na taarifa za miujiza kuendelea kutawala katika kanisa ikiwa mahubiri yatakuwa ni utajiri na uponyaji je mtu anapofanikisha hilo hitaji lake kuna haja yakumjuwa kristo?

Wakristo wengi wanashindwa kuyahamisha maisha yao kuwa yakikristo kulingana na taarifa chache walizonazo kuhusu Yesu wanacho kijuwa ni yesu ni mkombozi nakuliona jina lake nilenye nguvu na uwezo kama watu wataendelea kuwa kwenye mfumo huwo wa ukristo bandia usiofungamana na halisia ya kweli kama ilivyokuwa kwa yesu bado kanisa litakuwa na waaamini wengi katika tafsiri ya wingi.

Yesu aliishi kwajili yawengine je kanisani kuna watu wanaoishi kwajili ya watu wengine kulingana na mapokeo yalio tafsiriwa na manabii na mitume wanaoibuka leo duniani?

Bilashaka taswira ile iliyokusudiwa na Yesu bado haijaweza kufanikiwa kama tuna amini katika siku za mwisho tujitafakali endapo mwana wa adamu atakapo shuka sasa kwa maana haijulikani siku wala saa,

Je utakuwa katika nafasi gani kuingia peponi au jehanamu? tunaishi tafsiri ya kanisa nakushindwa kuishi maana ya ukristo maana iko katika matendo ya kila siku maana iko katika kuwa kama alivyokuwa Yesu.

Shetani ameshaingia kanisani anachokifanya nikuweka vitu kinyume na vile ambavyo inatakiwa mungu anatupa Baraka kila siku uzima anatupa kila wakati, lakini huwenda makanisa yanayo ibuka au mafundisho yanayotolewa yakawa hayana maana ya kanisa jinsi ilivyokusudiwa,